**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**


**Anuani ya simu "ELIMU"**
**Simu: 026 296 35 33**
**Barua pepe: info@moe.go.tz**
**Tovuti: www.moe.go.tz**

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya
S.L.P 10,
**40479 DODOMA.**


## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MABADILIKO YA TAREHE YA HAFLA YA UZINDUZI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 TOLEO LA 2023

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapenda kuwatangazia wadau wa Elimu na umma kuwa Hafla ya Uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, sasa itafanyika **tarehe 1, Febrauri, 2025** badala ya **tarehe 31 Januari, 2025**.

Kama ambavyo tulivyowatangazia umma hapo awali kupitia vyombo vya Habari, taarifa ya Msemaji Mkuu wa Serikali  na pia matangazo mbalimbali yanayoendelea hafla hii itafanyika katika ukumbi wa **Jakaya Kikwete Convention Center(JKCL)** na Mgeni Rasmi ni Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wakati akitoa taarifa ya mabadiliko hayo leo tarehe 30/01/2025 amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kukubali kuwa mgeni rasmi kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

Aidha, tunawakaribisha sana viongozi na wadau wote katika tukio hili la kihistoria Nchini.

Imetolewa na

Sylvia T. Lupembe
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**30 Januari, 2025**